

Bei ya maji Dar es Salaam

Je, wanaoendesa maghati ya maji wanazingatia bei walizopangia?



Utangulizi

Asilimia 38 ya kaya za mjini Dar es Salaam hupata maji kutoka kwenye visima na maghati ya maji, wakati asilimia 62 hutumia maji ya bomba. Asilimia 8 kati ya 62 wanapata maji ya bomba majumbani mwao, asilimia 38 wanapata maji ya bomba kwa majirani na asilimia 16 wanapata maji kwa kuyachota kwenye mabomba ya jumuiya, ambayo wakati mwingine hujulikana kama maghati ya maji (HBS 2007). Je, hawa watu waendao kwenye maghati ya maji kununua maji, huyanunua kwa bei gani?

Shirika la maji safi na maji taka DAWASCO ndilo pekee linalotoa huduma ya maji ya bomba jijini Dar es Salaam. Katika kuisimamia DAWASCO na ili kuhakikisha DAWASCO haitozi bei kubwa kupita kiasi, Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) hupanga bei ya kuuza maji. Kwa watu wenye mita binafsi, bei ya maji ni shillingi 0.637 kwa lita moja ya maji. Kwa wale wanaotegemea mabomba ya jumuiya au maghati ya maji bei ni shilingi 20 kwa kila lita 20, sawa na shilingi moja kwa lita.

Bei hii ilipangwa tarehe 10 Juni 2010 kupitia agizo la EWURA Na: 10-017. Katika agizo hilo hilo, EWURA Iliiagiza DAWASA, mmiliki wa maghati ya maji Dar es Salaam, kuhakikisha kuwa ifikapo tarehe 30 Juni 2010 bei mpya ziwe zimekwisha bandikwa katika kila ghati. Agizo hili la EWURA lilitolewa kwenye magazeti ya kitaifa nchini (Kielelezo na. 1).

Mwezi Agosti mwaka 2010, takriban wiki 4-6 baada ya agizo la EWURA kuanza kutekelezwa, Uwazi ilitembelea vioski 40 katika jiji la Dar es Salaam. Lengo lilikua kupata picha ya vioski, kufahamu bei za maji na kutathmini kama agizo la EWURA limetekelizwa.

Katika muhtasari huu, tunawasilisha mambo makuu manne yaliyothibitika katika ziara hizo. Kilichoonekana ni kuwa agizo la EWURA halifuatwi; bei rasmi iliyopangwa haikuwekwa hadharani au kubandikwa kwenye mbaa za matangazo; na maji yalikuwa yakiuzwa kwa bei ambayo ni mara saba zaidi ya bei rasmi iliyopangwa na EWURA.

Taarifa hizi zinaibua hisia za mashaka. Zinatuonesha kuwa maagizo ya mamlaka ya udhibiti yanapuuzwa, na kwamba gharama za maji kwa kaya zenyen hali duni ni kubwa mno ukilinganisha na gharama zinazolipwa na kaya zinazopata maji ya bomba moja kwa moja majumbani mwao. Waraka huu unahitimishwa na wito kwa mamlaka husika kuboresha usimamizi ili kuhakikisha kwamba maji ya bomba yanakuwa nafuu kwa wote.

Kielelezo na. 1: Agizo la EWURA namba 10-017 kuhusu bei ya maji katika maghati



In the matter of a Tariff Review by
"THE ENERGY AND WATER UTILITIES REGULATORY AUTHORITY" ("EWURA")
For a Tariff Adjustment for Standpipes/Kiosks in DAWASCO Operational Area

ORDER No.10-017 (Issued under Section 17 of the EWURA Act, CAP 414)

On 24th May,2010 residents of Kimara in Dar es Salaam raised complaints on high water charges which at times goes up to TZS 500 per 20lts bucket as compared to charges which were directed by DAWASCO of not more than TZS 20 per 20 liters bucket at Public Standpipes. The complaints were raised to the President of the United Republic of Tanzania during his tour in various Dar Es Salaam areas to inspect the situation of water supply services.

The tariff of TZS 20 per 20 liters which was directed by DAWASCO is equivalent to TZS 1,000 per cubic meter as against a tariff of TZS 637 per cubic meter (equivalent to TZS 12.37 per 20 liters bucket) which was approved by EWURA. The reason advanced by DAWASCO for not abiding to the approved tariff was that; the approved tariff of TZS 12.74 per 20 litre bucket is not practicable due to non availability of small currency denominations and therefore the tariff was rounded up TZS 20 per 20 liters bucket and the difference was retained by Standpipe Agents as a profit margin. EWURA found that there is a sense in rounding up to a tariff of which customers can easily get the currency for purchasing water in bucket units but observed that,DAWASCO was obliged to request for the tariff from EWURA. In view of the foregoing, it was obvious that a tariff review was necessary and therefore EWURA instituted the Inquiry process.

In the analysis of the tariff review, EWURA has taken into consideration, among other things, the terms in the Lease Agreement between DAWASA and DAWASCO, a letter from EWURA ref. EWURA/44/2/59 addressed to DAWASA and copied to DAWASCO, a reply letter ref. no. DAWASCO/DAW/35/VOL VII/292 from DAWASCO to EWURA and comments and clarifications provided during the consultation process.

A consultative process involving the Consumer Consultative Council (CCC) and the Government Consultative Council (GCC) took place on 2nd June 2010 and 3rd June 2010 respectively and on both meetings DAWASA and DAWASCO representatives were invited to provide clarifications.

Both CCC and GCC were of the opinion that, although a tariff of TZS 12.74 per 20liters bucket is not practicable, DAWASCO should have sought EWURAs approval before directing Standpipe customers to charge not more than TZS 20 for 20 liters bucket. Both CCC and GCC further recommended to EWURA, to round up and approve a tariff of TZS 20 per 20 liters bucket, which constitute readily available currency denominations. Furthermore, both CCC and GCC advised both DAWASCO and EWURA to monitor the tariff being charged at public Standpipes/ Kiosks. Lastly, the Consumers Consultative Council

advised EWURA to ensure that, in future, the approved tariff for a 20 liters bucket at public Standpipes/Kiosks is in readily available currency denominations.

As a result of the Inquiry, EWURA concluded that, the approved tariff by EWURA of TZS 12.74 per 20 liters bucket is not easily implementable.

The Board of Directors of EWURA having met on 8th June, 2010 to consider the tariff review for public Standpipes/Kiosks decided as follows;

- 1.0 The Board approves a water tariff of TZS 20 per 20 liters bucket /container at all public standpipes operated by DAWASCO with effect from 15th June 2010;
- 2.0 With effect from 15th June, 2010, DAWASA shall ensure that DAWASCO sets aside funds obtained from the difference between the old approved tariff of TZS 12.74 and the new tariff of TZS 20 per 20 liters bucket at Public Standpipes for the construction of Public Standpipes in Peri-urban areas;
- 3.0 On or before 30th June 2010, DAWASA shall ensure that DAWASCO presents the implementation plan for the construction of Public Standpipes referred to in item 2.0 to EWURA for approval;
- 4.0 DAWASA shall ensure that DAWASCO submits quarterly implementation reports of the project referred to in item 3.0 latest 30 days after the end of each quarter;
- 5.0 On or before 30th June 2010, DAWASA shall ensure that DAWASCO posts the approved tariff at each standpipe; and
- 6.0 On or before 30th June 2010, DAWASA shall ensure that DAWASCO signs agreements with local government authority in each locality having standpipes, so as to give them responsibility of making sure that Standpipes/Kiosks customers are not overcharged.

This Order shall take effect from 15th June 2010.

Dr. Geoffrey Mariki
Deputy Chairman of the Board
of Directors
EWURA

Haruna Masebu
Director General
EWURA

Dar es Salaam 8th June, 2010

Chanzo: Gazeti la The Citizen, la tarehe 10 Juni, 2010.

Jambo la 1: Maghati mengi ya maji hayafanyi kazi

Kwa ajili ya zoezi hili Uwazi ilichagua maghati 40 kutoka kwenye orodha ya maghati 185 yaliyoko Dar es Salaam. Maghati mengi kati ya haya yalioneckana kutofanya kazi, kwa maana kwamba hayatoi huduma ya maji. Kati ya maghati yote yaliyotembelewa, 25 yalikuwa yakifanya kazi na 15 yalithibitika kutofanya kazi kabisa. Wakati mwingine, maghati yaliyokuwa hayafanyi kazi yalikuwa yamegeuzwa kuwa mahala pa kutupia taka taka. Wakati mwingine maghati yalikuwa yamejengwa mahali ambapo upanuzi wa barabara ulikuwa ukiendelea.

Kielelezo na. 2: Baadhi ya maghati yasiyofanya kazi Dar es salaam



Keko Mwanga B



Jirani na Shule ya Sekondari
ya Loyola



Kigogo Luhanga Azimio St.

Hata katika maghati yaliyokuwa yakifanya kazi, utendaji haukuwa mzuri: Mara nyingi wauzaji hawakuwepo. Katika maeneo mengi ya wilaya ya Temeke, maghati yalikuwa yakifunguliwa nyakati za usiku tu muda ambao msukumo wa maji ulikuwa mkubwa kiasi cha kuweza kupampu maji.

Ziara hizi pia zilibaini kuwa idadi kubwa ya maghati yalikuwa yamekodishwa kwa wafanyakishara wakilipa pango la kila mwezi kwa Serikali za Mitaa. Hii inaweza kuleta mgongano wa maslahi kwa sababu kulingana na agizo la EWURA, ni jukumu la Serikali za Mitaa kusimamia bei ya maji kwenye maghati :

"Ifikapo tarehe 30 mwezi Juni mwaka 2010, DAWASA itahakikisha kuwa DAWASCO imesaini makubaliano na Serikali za Mitaa katika maeneo yenye maghati/vioski vya maji ili kuwapa jukumu la kuhakikisha kuwa wateja hawatowwi zaidi ya bei iliyopangwa.


Agizo la EWURA na. 10-017." (tafsiri yetu)

Jambo la 2: Matangazo ya bei rasmi hayakubandikwa

Agizo la EWURA na. 10-017 lilitangaza bei mpya ya maji kwa wanunuzi wa maji katika sehemu zenye maghati ya maji. Pia, liliisema kwamba:

"Ifikapo tarehe 30 mwezi Juni mwaka 2010, DAWASA itahakikisha DAWASCO inaweka matangazo ya bei mpya katika kila ghati." (tafsiri yetu)

Kielelezo Na. 3: Matangazo ya bei mpya kwenye vioski vya maji




Tip Top

Ubungo Maziwa

Kati ya maghati 25 yaliyokuwa yakifanya kazi ni mawili tu, Ubungo Maziwa na TipTop, ndiyo yaliyozingatia agizo hili. Maghati mengi hayakubandika matangazo yanayoonyesha bei mpya. Hata hivyo, pamoja na kwamba agizo la bei mpya libibandikwa Ubungo Maziwa na TipTop, maeneo hayo yalitoza bei kubwa kuliko iliyopangwa. Ubungo Maziwa iliwakataa wateja walioataka kununua maji kwa bei ya shilling 20 kwa kila ndoo. Badala yake maji yaliuzwa kwa shilingi 100 kwa ndoo ya lita 20 kwa wale waliokulaliana na bei hiyo. Eneo la TipTop ndoo ya lita 10 na ile ya lita 20 ya maji ziliuzwa kwa bei sawia ya shilingi 30 kwa ndoo.

Kielelezo na. 4: Maghati ya maji yasiyofuata agizo la EWURA la kubandika bei rasmi (n=25)



Jambo la 3: Maghati yote yalitoza bei kubwa kuliko bei rasmi

Agizo la EWURA linatamka bayana kuwa:

"Bodi imepitisha bei rasmi ya maji ya shilingi 20 kwa kila ndoo ya lita 20 katika maghati yote yanayosimamiwa na DAWASCO kuanzia tarehe 15 Juni mwaka 2010." (tafsiri yetu)

Hakuna ghati hata moja kati ya maghati 25 yaliyokuwa yakifanya kazi katika sampuli yetu lililotoza bei hii. Yote yalitoza zaidi na baadhi yalitoza bei kubwa kupita kiasi.

Kielelezo na. 5: Bei ya maji iliyotangazwa kwenye maghati tofauti




Tandale kwa Tumbo

Keko Magurumbasi

Bei ya chini kabisa iliyodaiwa kwa lita 20 ilikuwa ni shilling 30, na hii ilikuwa katika maghati mawili tu, Tip Top na Keko Magurubasi. Ingawa maghati haya yalitoza asilimia 50 zaidi ya bei rasmi, haya ndiyo yalikuwa yakitoza bei ya chini zaidi ukilinganisha na maghati mengine yaliyotembelewa na Uwazi.

Bei iliyofuata kwa unafuu ilikuwa ni shilingi 50 kwa ndoo iliyotozwa na maghati matano. Aidha, upande mwengine wa wigo maghati 10 kati ya 25 yalitoza shilingi 150 kwa kila ndoo ya lita 20 (zaidi ya asilimia 650 ya bei rasmi), na ghati moja lililopo Manzese Bakhresa limefikia hadi kutoza shilingi 200 kwa kila ndoo.

Kielelezo na. 6: Bei zilizotozwa na maghati mbali mbali kwa ndoo ya maji ya lita 20




Jambo la 4: Maji yanayochotwa kwenye ndoo za lita 10 yanagharimu kiasi kikubwa zaidi

Kwa kupanga bei ya shilingi 20 kwa ujazo wa lita 20, inategemewa kwamba maji katika maghati hayatogharimu zaidi ya shilingi moja kwa kila lita.

Agizo la EWURA, hata hivyo, halizungumzii maji yanayochotwa katika ujazo mdogo zaidi. Hii inaweza kuwa ni usahafulifu kwa vile watu wengi hupendelea kuchota maji katika ujazo wa lita 5 na 10 kwa sababu hubebeka kirahisi zaidi. Maghati mengi yameonekana kuwa na bei tofauti kwa wachotaji wa maji kwenye ndoo za lita 10. Kama kielelezo namba 7 kinavyotuonyesha, maji haya ni ghali zaidi kuliko maji yanayochotwa kwenye ndoo za lita 20.

Kwa watu wanaochota maji kwa kutumia ndoo za lita kumi, maji ni ghali mno. Zaidi ya nusu ya maghati yaliyotembelewa na Uwazi, yameonekana kutoza kiasi cha shilingi 10 kwa lita, ambayo ni mara 10 ya bei iliyopangwa na EWURA. Katika ghati linalotoza bei nafuu zaidi, Keko Magurumbasi, wateja wake walinunua lita 10 za maji kwa bei ya lita 20: yaani shilingi 20.

Kielelezo na. 7: Bei kwa lita iliyotozwa kwa vyombo vyenye ujazo wa lita 10 na lita 20



Hitimisho

Muhtasari huu umezingatia bei za maji zilizotozwa katika sampuli ya maghati 25 yaliyochaguliwa bila mpangilio maalum katika jiji la Dar es Salaam. Utafiti umeonyesha kuwa bei rasmi iliyopangwa na EWURA ya shilingi 20 kwa ujazo wa lita 20 za maji haizingatiwi. Hakuna hata moja katika maghati yaliyotembelewa ambalo lilikuwa likitoza bei hii, na mengi yalikuwa yakitoza bei ambazo ni mara saba au hata mara kumi zaidi ya bei rasmi.

Ziara zilizofanyika zimebainisha mambo ya ziada yanayoleta mashaka. Maghati mengi hayafanyi kazi ama yanafunguliwa kwa muda mchache. Iligundulika kwamba serikali za mitaa ambazo zimepewa jukumu la kusimamia bei rasmi iliyopangwa na EWURA, zinakabiliwa na mgongano wa maslahi kwa kuwa baadhi yake zimekodisha maghati hayo kwa waendeshaji ambao wanahitaji kutoza bei kubwa zaidi ili waweze kufidia gharama ya pango la maghati wanayolipia. Aidha, wateja wengi walipendelea zaidi au waliweza kumudu kununua maji katika ujazo wa lita 5 au lita 10, viwango ambavyo havikupangiwa bei rasmi .

Ni jambo la kukatisha tamaa kuona kwamba agizo la EWURA linapuuuzwa kwa kiasi hiki. Maji safi kwa gharama nafuu ni hitaji la msingi kabisa na ni muhimu kwamba Serikali za Mitaa zenye jukumu la kuhakikisha kwamba maagizo ya EWURA yanatekelezwa wafanye kazi yao. Mpaka hapo watakapofanikiwa kufanya hivyo, EWURA wenywewe inaweza kulazimika kuisimamia DAWASCO kwa makini zaidi ili kuhakikisha maji ya bomba yanapanikana kwa gharama nafuu.

Kielelezo na. 8: Kioski eneo la Manzese Uzuri



Kiambatisho: Vioksi vilivyo tembelewa, na bei ya maji katika vioski hivyo

Jina la eneo	Bei kwa lita 20	Bei kwa lita 10	Tangazo
Mabibo Kwa Cassian	50	30	Hapana
Mabibo kwa Kikanzo	100		Hapana
Keko Magurumbasi B	30	20	Hapana
Keko Mwanga A	50	30	Hapana
Keko Molemo	50	30	Hapana
Kigogo Landa Bar	70	40	Hapana
Mabibo Relini	50	50	Hapana
Ubungo Maziwa	100		Ndiyo
Tandale Uzuri	150	100	Hapana
Tandale kwa Tumbo	150	100	Hapana
Tandale Yemen	150	100	Hapana
Mkunduge	100	50	Hapana
Mtogole	100	50	Hapana
Ali Maua	100	50	Hapana
Manzese Uzuri	150	100	Hapana
Ali Maua	50	30	Hapana
Tandale Mafichoni	150	100	Hapana
Mivuleni	150	100	Hapana
Mwembe Mkole	150	100	Hapana
Mivuleni	150	100	Hapana
Manzese Bakhresa	200	100	Hapana
Manzese Kilimani	150	100	Hapana
Manzese Midizini	100	50	Hapana
Manzese Kiembeni	150	100	Hapana
Tip Top	30	30	Ndiyo

Chanzo: Utafiti wa Uwazi kuhusu Maghati ya maji.